# Kenya Inapaswa Kutoa Maelezo Kuhusu Waliotoweka Katika Operesheni ‘Okoa Maisha’

***Mahakama Ya Kimataifa ya Uhalifu Ipanue Uchunguzi Wake Ili Ujumuishe Pambano La Mlima Elgon***

(Nairobi, Tarehe 27 Oktoba mwaka wa 2011) – Zaidi ya watu mia tatu hawajulikani waliopo miaka mitatu baada ya hatua za kuwasaka waasi zililizochukuliwa na serikali katika eneo la Mlima Elgon. Kulingana na ripoti iliyotolewa leo na shirika la haki za binadamu, Human Rights Watch, idadi kubwa ya watu hawa walitoroshwa kwa nguvu na Jeshi la Kenya.

Serikali ya Kenya inapaswa kuunda tume huru mara moja ambayo itayafukua maeneo yanayokisiwa kuwa makaburi ya halaiki na kuchunguza pia uhalifu uliotendwa na maafisa wa usalama wa Kenya na waasi wa Sabaot Land Defence Force (SLDF). Aidha Mahakama Ya Kimataifa Ya Uhalifu (yaani ICC) inapaswa kupanua uchunguzi wake nchini Kenya ikiwa serikali ya Kenya haina uwezo ama haitaki kufanya chunguzi hizi.

Ripoti hii yenye kurasa 48 inayoitwa, “‘Funga Roho’: Kutafuta Haki Katika Eneo La Mlima Elgon Nchini Kenya” inaangalia kwa undani hatua za kutafuta ukweli na haki zinazochukuliwa na familia za wale ambao walitoroshwa kwa nguvu na Jeshi la Kenya pamoja na kundi la SLDF.

Shirika hili la Human Rights Watch lilisema kwamba serikali ya Kenya imewasaidia waathiriwa katika harakati hizi kwa kiwango kidogo katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita. Vile vile serikali haijahakikisha kuwa uchunguzi huru na usiopendelea upande wowote umefanywa kuhusu madai ya ukuikaji wa haki za binadamu uliofanywa na jeshi na kundi la SLDF.

“Hali mbaya ya familia za waathiriwa ni mojawapo za kovu za ghasia za Mlima Elgon,” alisema Daniel Bekele, mkurugenzi kwa Idara ya Afrika katika shirika la Human Rights Watch. “Bila maiti ya kuzika, bila vyeti vya vifo, na bila njia yoyote rasmi ya kudhihirisha kwamba waliwapoteza wapendwa wao, familia hizi hawana pa kwenda.”

Ripoti hii inatokana na uchunguzi pamoja na mahojiano yaliyofanywa katika Mkoa wa Magharibi ya Kenya. Ingawa kuna visa vingi vya ukiukaji wa haki za binadamu katika eneo la Mlima Elgon ambavyo havijachukuliwa hatua za kisheria, ripoti hii inaangazia tu maswala mawili maalum. Lile la kwanza ni utekaji nyara na kundi la SLDF na la pili ni kutoweka kwa wale waliokuwa mikononi mwa maafisa wa usalama wa Kenya.

Shirika la Human Rights Watch lilisema kuwa serikali ya Kenya inapaswa kuwa ya kwanza katika kuchunguza uhalifu uliofanywa katika eneo la Mlima Elgon na kama ripoti hii inavyoonyesha, uchunguzi wa kuaminika haujafanywa katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita.

Uasi ulianza mwaka wa 2006 wakati ambapo kundi la SLDF lilikataa hatua za serikali za kuwafurusha maskwota. Jeshi la waasi hawa liliwashambulia maelfu ya raia

walioshukiwa kwamba waliiunga serikali mkono katika shughuli hii huku wakiwabaka, wakiwaua na kuwakata wengine viungo vya mwili. Uchaguzi wa Disemba mwaka wa 2007 ulipokaribia, kundi la SLDF liliwafanyia kampeni wagombea viti vya udiwani na ubunge wa chama cha upinzani cha Orange Democratic Movement (ODM) kwa kuwatisha wapiga kura.

Kutokana na visa hivi, mnamo Machi mwaka wa 2008, serikali ya Kenya ilianzisha operesheni kali iliyojumuisha jeshi na polisi. Operesheni hii ilijulikana kama “Okoa Maisha” na maafisa wa usalama waliwaua mamia ya watu kinyume na sheria pamoja na kuwatesa wengine na kuwazuilia maelfu kiholela.

Kundi la SLDF liliwaua watu karibu mia saba na hamsini kati ya mwaka wa 2006 hadi katikati ya mwaka 2008. Nao maafisa wa usalama waliwaua karibu watu mia mbili na sabini katika kipindi hiki. Vile vile inasemekana kuwa karibu watu mia tatu walitoweka. Kama mia moja tisini na tisa walitoweka wakiwa mikononi mwa maafisa wa usalama ilhali mia moja ishirini na sita wakiwa mikononi mwa SLDF.

Mwanamke mmoja alielezea alichoambiwa na wanajeshi walipomchukua mumewe: “Umeisikia milio ya risasi katika eneo la Kimaswa? Hiyo ndiyo silaha ambayo itatumiwa kwa mumeo.”

Unyama wa SLDF katika eneo la Mlima Elgon pamoja na jeshi kutumia nguvu nyingi kupita kiasi katika kukabiliana nao ulimalizika katikati ya mwaka wa 2008 baada ya kumulikwa na mashirika yanayotetea haki za binadamu ya kitaifa na yale ya kimataifa. Baada ya kumulikwa, jeshi na polisi walidai kuwa wanafanya uchunguzi wa ndani kuhusu tabia za makundi yaliyohusika. Mwishowe waliyapuuza madai ya ukiukaji wa haki za binadamu na hakuna afisa yeyote wa usalama ambaye alichukuliwa hatua za kinidhamu.

Licha ya idadi kubwa ya mauaji yaliyotekelezwa na kundi la SLDF pamoja na ukweli kwamba zaidi ya wanaume na wavulana elfu tatu walikamatwa na kuzuiliwa na maafisa wa usalama kwa kushukiwa kuwa ni wanachama au wanaliunga mkono kundi la SLDF, ni wanne tu waliopatikana na hatia ya kuua kwa bahati mbaya au bila kukusudia ilhali wengine wao walishtakiwa kwa makosa madogo madogo kama kuwa wanachama wa kundi haramu. Mamia ya mauaji, kutoroshwa kwa wengine, kesi za ubakaji na mateso yaliyofanywa na kundi la SLDF katika eneo la Mlima Elgon kwa niaba ya wanasiasa hazikuhukumiwa.

Kwa sababu hakuna uchunguzi wa kuaminika wa kitaifa uliofanywa, shirika la Human Rights Watch linapendekeza kuwa mwendesha mashtaka katika Mahakama Ya Kimataifa Ya Uhalifu (ICC) achunguze kama uhalifu chini ya mamlaka ya ICC ulifanywa katika eneo la Mlima Elgon na baadaye afanye uchunguzi zaidi nchini na awachukulie hatua wale watakaopatikana na hatia kubwa zaidi. ICC tayari inafanya uchunguzi nchini Kenya kufuatana na ghasia za baada ya uchaguzi wa rais uliotokea mwaka wa 2007.

Ni lazima serikali ya Kenya itimize wajibu wake wa kuilinda haki za raia wake wote," alisema Bekele. "Ikiwa haiwezi kutekeleza haki kwa waathiriwa wa eneo la Mlima Elgon ambao familia zao zimengojea haki kwa zaidi ya miaka mitatu, basi mashirika mbalimbali ya kiafrika na yale ya kimataifa yaingilie kati swala hili."

Serikali pia haijachukua hatua madhubuti ya kuyatafuta na kuyafukua makaburi ya halaiki ili kuiruhusu maiti ile kuzikwa kwa njia ya heshima, shirika la Human Rights Watch liliongezea. Baadhi ya makaburi yalifukuliwa wakati wa operesheni ya kijeshi ya mwaka wa 2008 na wakazi wa Mlima Elgon wanasema kwamba kuna mengine mengi ambayo hayakufukuliwa. Na mashirika madogo yasiyo ya kiserikali yanayofanya kazi katika eneo hili la Mlima Elgon yalitishwa na wanajeshi yalipojaribu kuyatafuta makaburi mengine.

Isitoshe maafisa wa serikali wamewazuia familia za waliotoroshwa kupata fidia hatua ambayo ingewapa nafasi ya kuthibitisha rasmi kwamba waliwapoteza jamaa zao. Mashirika ya wajane na jamaa za waathiriwa waliliezea shirika la Human Rights Watch kuwa hawawezi kupata vyeti vya vifo vya jamaa zao ambao hawajapatikana hadi leo hivyo basi hawawezi pia kupata fidia au msaada wowote kulingana na sheria za Kenya kama vile hati za umilikaji wa ardhi, mali mengine na hata pesa katika benki.

Mawakili na mashirika yanayotetea haki za binadamu yamewasaidia waathiriwa kuwasilisha kesi katika Mahakama Kuu Ya Bungoma au yamewasilisha kesi kwa niaba yao katika Mahakama Ya Haki Ya Afrika Mashariki (East African Court of Justice).Wengine wamepeleka malalamiko kwa Tume Ya Afrika Juu Ya Haki za Binadamu na Watu (African Commisssion on Human and People's Rights). Baadhi ya mawakili na mashirika haya pia yamewasilisha malalamiko mbele ya Kikundi cha Umoja wa Mataifa Kinachofanya Kazi Juu Ya Waliotoroshwa (United Nations Working Group on Enforced or Involuntary Disappearances).

"Serikali ya Kenya inapaswa kukubali kuwa idadi fulani ya watu walitoroshwa kisha ichukue hatua inayofaa kufukua makaburi ya halaiki na kuwatambua waathiriwa," Bekele alisema. "Kenya imezinyima ukweli na haki familia za waathiriwa na kuwazuia kupata misaada mingine kwa kutochukua hatua hizi."

**"'Funga Roho': Kutafuta Haki Katika Eneo La Mlima Elgon Nchini Kenya," inapatikana hapa:** http://www.hrw.org/reports/2011/10/21/hold-your-heart

**Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:**
Nairobi, Ben Rawlence (Kiingereza, Kiswahili): +254-725-369-652; or + 44-79-8481-6013 (rununu); au rawlenb@hrw.org
Nairobi, Neela Ghoshal, (Kiingereza, Kifaransa): +254-729-466-685 (rununu); au ghoshan@hrw.org
New York, Daniel Bekele (Kiingereza, Kiamhari): +1-212-216-1223; or +1-917-385-3878 (rununu); au bekeled@hrw.org

**Baadhi ya Ushahidi Kutoka Kwenye Ripoti " Funga Roho"**

Mnamo tarehe 16 Machi, mwaka wa 2008, mume wa Faith V. alikamatwa na wanajeshi kutoka nyumbani kwao:

> Walianza kumtesa mume wangu kando ya nyumba yetu. Walikuwa wanajeshi kutoka Chepkube. Na nilipoona jinsi alivyopigwa, niliwafungia watoto wetu ndani ya nyumba ili wasimwone. Singaliweza kuvumilia… niliamua kukimbia hadi ndani ya nyumba ili nisimwone tena.
>
> Nilipoanza kulia, watoto nao walianza kulia jambo lililowafanya wanajeshi wamrudishe ndani ya nyumba halafu aliwaonyesha kitambulisho chake. Waliniambia "Tumemrudisha ili umwone kwa mara ya mwisho. Umezisikia zile risasi za Kimaswa? Hizo ndizo silaha ambazo zitatumiwa kwa mumeo." Mume wangu alishukiwa na wanajeshi kwa sababu anatoka katika eneo la Chepyuk. [Eneo hili ni lile ambalo wakazi walikuwa wamefurushwa kutoka na serikali hatua ambayo ulipingwa na kundi la SLDF.]

Elsa Chesut, mume wake hakuonekana tena baada ya msako uliofanywa na wanajeshi:

> Mnamo tarehe 20, niliamua kwenda kumtafuta mume wangu kwenye kambi ya wanajeshi alipokosa kurejea nyumbani. Niliambiwa na askari mmoja katika lango la kambi kuwa, "Waume hawatafutwi kambini ila wanatafutwa msituni. Nenda kamtafute mume wako msituni. Mwanajeshi yule alinijibu kwa sababu jumba la kuhifadhia maiti lilikuwa msituni na ni kule ndiko miili ilitupwa. Lakini kwa wakati ule sikufikiria kwamba angekufa. Sikuamini kwamba alikufa.

Jane A. alilielezea shirika la Human Rights Watch kuhusu mtoto wake wa kiume aliyetekwa nyara na SLDF:

> Sijawahi kuripoti kwa serikali kuhusu mwanangu. Sijui njia ya kufuata. Na sikujua tofauti kati ya majambazi na polisi.

Maelezo kutoka kwa mwanamke ambaye mume wake alitekwa nyara:

> Sikuenda kwa chifu wala polisi kwa sababu ningalienda, ningaliuawa. Niliogopa kuwa kwa kuripoti ningalihatarisha maisha yangu. Na sijawahi kuripoti hadi leo kwa sababu bado ninaogopa. Wafuasi wa SLDF wangali msituni hata wengine wao wameachiliwa na mahakama na wako miongoni mwetu na mtu anaweza kuuawa tu kwa kulitaja jina lao.

Ursula C., mume wake alitoroshwa na jeshi na kumwacha na watoto tisa naye pia aliongea na shirika la Human Rights Watch:

> Ninawalea watoto hawa kwa shida nyingi. Nilikuwa na watoto wawili katika shule ya sekondari na nilishindwa kuwalipia karo na hata shule haingeweza

kunisaidia kuwalipia karo bila hati ya kifo cha mume wangu. Nilipoenda kwa chifu kutafuta hati hii, aliniambia, “ Hujamzika mume wako. Unataka nifungwe jela? Una ushahidi gani ya kuonyesha kuwa mume wako alikufa? Umejuaje kuwa alikufa? Labda ameenda Uganda au pahali pengine.” Mwishowe alinifukuza nami nikaamue kumwuza ng’ombe mmoja aliyebaki ili niwalipie karo.